

TAHADHARI YA UNABII!

Masihi Anakuja

Maono ya Mei 4, 2014

Katika usiku wa Mei tarehe 4, mwaka wa 2014, BWANA Alinena nami katika njia ya ajabu na ya kipekee sana ambapo niliona

maono makuu ya MUNGU juu ya matukio yalio karibu kutendeka. Katika maono hayo, ghafla, BWANA Alinipeleka mahali ambapo Aliniuliza nikatazame juu angani. Nilipotazama juu angani, nilistaajabu sana kushuhudia UTUKUFU mzito sana WA BWANA, kama jua la siku angavu ya majira ya kiangazi. Lakini, nilipokuwa nikiangalia juu angani, niligundua kwa haraka kwamba UTUKUFU WA BWANA uliokuwa ukija kwa hakika *uling'aa* kwa *ukali* mkuu sana na *uwezo* kutoka mbinguni kuelekea chini duniani. UTUKUFU Niliyouona *ukimetameta* kutoka mbinguni uliangaza mifumo ya miali ya utukufu iliotoka kwa BWANA mbinguni. Ile miali ya UTUKUFU ilikuwa ya kumetameta sana kiasi kwamba singeweza kuitazama kwa macho yangu. Huo UTUKUFU WA MUNGU uliotoka mbinguni ulikuwa wa *nguvu* sana kiasi ya kwamba ulijaa katika anga yote. Miali ya UTUKUFU ilijitokeza kwa ukali mzito sana kiasi ya kwamba *iliangazia* dunia nzima kihalisia. Huo UTUKUFU WA MUNGU ulioangaza kuelekea dunia ulikuwa katika *miali* ya utukufu ya kumetameta iliotengeneza umbo *kama mduara* juu ya anga yote na kufunika mpaka miisho ya dunia. Nilipoona jinsi miisho ya hiyo *miali* ya UTUKUFU iligusa upeo wote wa dunia Kotekote, ndipo nikatambua kwamba hakuna kiumbe chochote kilicho hai hapa duniani kitahepa

hili tukio. Hapo ndipo mahali ambapo Sauti Ilinena kutoka mbinguni ikisema,

“TAZAMA, MASIHI ANAKUJA.”

Wakati huo, nilipotazama upande wangu wa kushoto, Niliona UTUKUFU MKUU WA BWANA *ukiangaza kama radi* kutoka angani kuelekea upande unaoangalia mashariki. *Kuangaza* kwa UTUKUFU Mkuu WA BWANA niliona ilitendeka *ghafla kwa kufumba na kufumbua jicho*. Baada ya UTUKUFU *kumulika* mara mbili kama *radi* katika upande wa mashariki, ninakumbuka vyema kabisa kwamba BWANA Alinisababisha nijue kwamba kanisa huko nje kwa hakika HALIKUWA TAYARI; hata MASIHI Alipokuja! Katika hayo maono makuu, Kwa hakika BWANA Alinitetemsha Alipoomboleza kwamba kanisa ambalo halikuwa limejiandaa liliukosa *unyakuzi*. Hapo ndipo BWANA Alinisababisha nijue jinsi Alivyokuwa na huzuni mwingi sana katika moyo WAKE ya kwamba kanisa halikuwa tayari wakati wakuja kwake Masihi. BWANA YEHOVA wakati huo Aliupitiza huzuni WAKE katika moyo wangu na nikahisi *ghamu* ya moyo WAKE kiasi ya kwamba singeweza kustahimili tena! Hiyo ndio iliyonisababisha kuvunjika, na kulia kwa uchungu huku nikijitupa chini mara kwa mara! Bado ninakumbuka vyema kabisa kwamba niliendelea kulia bila kukoma huku nikisaga meno yangu, kwa muda mrefu sana ardhini! Katika maono hayo, BWANA Alinisababisha nikajue papo hapo kwamba sababu ambayo kanisa halikuwa tayari ni

kwa sababu halikuwa limeyatoa maisha yake katika utakatifu, na pia halikuwa limekumbatia uhaki wake usiokwisha. Kile kilichojitokeza wazi wazi kutoka katika maono haya ni swala kwamba nimesikia SAUTI YA MALAIKA MKUU MWENYEWU kwa sauti Akitangaza KUJA KWA MASIHI. Hata hivyo, hatupaswi kuwahi kupoteza ufahamu wa swala kwamba BWANA Anasema kuwa hivi karibuni kutakuwa na tukio kuu ajabu ambalo litafanyika *ishara kuu na ya ajabu* kuwahi kushuhudiwa duniani. Tukio hili litatendeka angani juu ya ardhi na litashangaza ulimwengu mzima katika njia ile ambayo haijawahi kuonekana kamwe. Ningependa kusema kuwa, BWANA Amehuzunika na hali ya *kutojiandaa* kwa kanisa. Kwa maneno mengine, Anasema kwamba bado kanisa si komavu, bado haliko kamilifu, bado halijakuwa bila doa, bado si lenye bila alama, bado halijakuwa bila kunyanzi, kuweza kuingia katika Ufalme WAKE. Nilipoamka, Nilitetemeka na kulihuzunikia sana kanisa kwa maana tayari nimekwisha ona wengi wakikosa *unyakuzi* na wakilia huku wakisaga meno yao na kujitupatupa ardhini. Kwa maana huyu ndiye YEYE, ambaye habari zake zimeandikwa,

“Tazama namtuma mjumbe mbele yako, atakayetengeneza njia mbele yako. (Mathayo 11:10) ■